



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATA 14 ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa kata kumi na nne (14) Tanzania Bara kuwa kutakuwa na **Uchaguzi Mdogo wa Madiwani siku ya Alhamisi, tarehe 13 Julai, 2023**. Kata zinazofanya Uchaguzi ni Ngoywa, (Sikonge DC), Sindeni (Handeni DC), Kalola (Uyui DC), Kalemawe na Njoro (Same DC), Magubike (Kilosa DC), Mahege (Kibiti DC), Kinyika (Makete DC), Mbede (Mpimbwe DC), Bosha (Mkinga DC), Kwashemshi (Korogwe DC), Bunamhala (Bariadi TC), Mnavira (Masasi DC) na Potwe (Muheza DC).

1. **SIKU:** Wananchi watapiga kura siku ya Alhamisi tarehe 13 Julai, 2023
2. **VITUO:** Upigaji kura utafanyika katika vituo vilivyotumika wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 1:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 10:00 kamili Jioni

Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi

1. Mpiga kura anatakiwa kwenda katika kituo alichojiandikisha na kadi yake ya mpiga kura siku ya uchaguzi.
2. Wapiga Kura waliopoteza kadi zao za kupigia kura au zilizoharibika, wanaruhusiwa kutumia vitambulisho mbadala kimojawapo kati ya:-
 - a) Hati ya kusafiria,
 - b) Leseni ya Udereva, na
 - c) Kitambulisho cha Taifa

Majina yote matatu yaliyomo katika vitambulisho mbadala yafanane na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

3. Mpiga kura akifika kituoni anatakiwa kupanga mstari.
4. Mpiga kura anatakiwa kufuata maelekezo yote atakayopewa na msimamizi wa kituo.
5. Mpiga kura awapo kituoni anatakiwa kutoa kipaumbele kwa wapiga kura wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenyeu ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokuwa nao kituoni.
6. Watu wenye mahitaji maalum wanaruhusiwa kwenda kituoni na msaidizi.
7. Ifikapo muda wa kufunga kituo saa 10:00 kamili Jioni kama wapiga kura bado wapo kwenye mstari, mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mtu wa mwisho na zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wapiga kura walio kwenye mstari watakapomalizika. Mpiga kura atakayefika zaidi ya muda wa kufunga kituo hataruhusiwa kupigia kura.
8. Baada ya kumaliza kupigia kura, mpiga kura anatakiwa kuondoka eneo la kituo cha kupigia kura.

Kumbuka kupiga kura ni haki yako ya msingi jitokeze siku ya uchaguzi ukachague Diwani unayemtaka.

Emmanuel Kawishe
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI